

**OFISI YA RAISI  
TAWARA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA MTAMA**

**SHULE YA SEKONDARY MKOPWE**

**SLP. 235**

**MTAMA-LINDI**

**15.12.2020**

**KUMB N1 MTDC/MKSS/FMI/ADM/VOL1/20**

**JINA LA MWANAFUNZI : .....**

**SHULE ATOKAYO : .....**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

1. Ninayo furaha kukuarifu na kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka wa masomo unaoanza January .....
2. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/20....., unatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa siku hiyo. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa atakayeshindwa kuripoti shuleni tarehe iliyotajwa hapo juu .
3. Masomo utakayojifunza ni  
Civics, History, Geography, English, Ekiswahili, Physics, Chemistry, Biology na Basic Mathematics.  
Masomo yote yatafundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili .
4. Utakuwa unatumia lugha ya kiingereza muda wote uwapo hapo shuleni .
5. Nafasi hii uliyoipata ni muhimu sana kwako na Taifa kwa ujumla hivyo unatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa na kwamba utatumia muda wako, akili zako na maarifa kwa kushirikiana na wanajumuiya wa shule hii ili kuwezesha kupata Elimu , ambayo ndiyo kitu kikubwa na pekee kilichokuleta shuleni .  
Ni matumaini yangu kuwa utayatekeleza na kuzingatia mambo yote ili kurahisisha utoaji wa taaluma.
6. **TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO NA MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU .**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII :**

.....  
*Zainabu S. Mataka*  
**ZAINABU S. MATAKA**

## **MAHITAJI MUHIMU YA SHULE**

### **1. SARE ZA SHULE**

#### **A: WASICHANA**

- Sketi pea mbili ,rangi ya kijani ,aina ya kitambaa ni kitambaa kizito cha suti (Namba 1 )mshono wa linda box iwe ndefu.
- Blauzi iwe nusu kanzu mikono iwe nyeupe ,ndefu iliyobana mabega , ziwe pea mbili
- Shati nyeupe mikono mifupi,pea mbili kwa wale wasio vaa hijabu .
- Viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi pea mbili .
- Soksi nyeupe pea mbili.
- Leso (kitambaa cha mkononi )

#### **B:WAVULANA:**

- suruali pea mbili , rangi ya kaki,mshono wa celebration linda mbili upande wa kulia na upande wa kushoto na "MODO NI MARUFUKU"
- sharti nyeupe mikono mifupi pea mbili
- viatu nyeusi vya ngozi pea mbili
- soksi nyeupe pea mbili
- leso (kitambaa cha mkononi)
- mkanda mweusi wa ngozi usio na DSM ya madoido

ANGALIZO:Sare lazima ziwe za staha na heshima sawa na maadili ya kitanzania.Msichana sketi lazima iwe ndefu sio juu ya magoti na mvulana suruali yake isiwe modo na sehemu ya chini lazima ifunike visigino vya viatu vyake ikiwa imekaa kisawa sawa kiunoni mwake visigino vya viatu vyake ikiwa imekaa kisawasawa kiunoni mwake .

TAFADHARI :MZAZI SIMAMIA USHONAJI WA SARE ZA SHULE ZA MTOTO.

### **2:VIFAA VYA TAALUMA :**

- daftari kubwa (counter books )10
- peni ,penseli,rula na vifutio
- mkebe 1.
- Rim moja ya karatasi
- Dictionary ya kiingereza
- Begi la kuhifadhia /kubeba vifaa hivyo
- Faili moja la plastistic au Tsh 2000/=
- Passport size tatu

